# FRONTRUNNER EXAM
## DARASA LA TANO MWAKA2021 ⟨5⟩
## KISWAHILI

FRONTRUNNER 007

**Time: 1 Hour 40 Minutes**

**KISWAHILI** **Muda: Saa 1 Dakika 40**

**SEHEMU YA A: LUGHA**

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa karatasi hii ya maswali na karatasi ya kujibia. Karatasi hii ina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika karatasi hii
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika karatasi hii ya maswali.

***Soma taarifa ifuatayo kisha uchague jibu sahihi***

Kuna aina mbalimbali za michezo duniani. Michezo ___1___, ___2___ na wanaume na pia wanawake. Wanaume ___3___ zaidi soka, miereka na ndondi, ___4___ wanawake hupendelea zaidi mpira wa wavu au wa magongo. Tofauti kubwa ni kwamba michezo wanayopendelea wanaume ni ___5___ ___6___ hutumika nguvu. Wanawake ni nadra kupendelea mchezo ___7___ hutaka matumizi ya nguvu. Katika michezo yote, ___8___ huvaa sare ___9___ rangi aina moja kuwatambulisha. Kila mchezaji ana nambari ___10___ kuonyesha yeye ni nani na anacheza kama nani.

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| 1. | wenyewe | yenyewe | zenyewe | lenyewe |
| 2. | hucheza | huchezea | huchezesha | huchezwa |
| 3. | hupendeza | hupendezea | hupendelea | hupendekeza |
| 4. | ilhali | kumbe | labda | pengine |
| 5. | ule | yale | zile | ile |
| 6. | ambayo | ambazo | ambavyo | ambao |
| 7. | ambayo | ambazo | ambavyo | ambao |
| 8. | mchezaji | mchezi | wachezi | wachezaji |
| 9. | zenye | yenye | wenye | lenye |
| 10. | yenye | zenye | wenye | lenye |

Hapo awali ___11___ ya ___12___ kwa wageni wowote katika bara ___13___ la Afrika, watoto walikuwa na tabia ___14___ sana. Sasa kwa nini tuache mkondo ___15___ asilia na kuiga mambo yaliyokuja na wageni ambayo hayatufai?

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| 11. | mbele | nyuma | kabla | mbali |
| 12. | kuja | kukuja | hawajaja | waje |
| 13. | hii | huu | hili | hapa |
| 14. | jema | mwema | mzuri | njema |
| 15. | hiyo | huo | huyo | hilo |

16. "Sango hatakuja" Sentensi hii ni ya wakati upi?

A. ujao B. uliopita

C. uliopo D. timilifu

17. Mtu aliye na nundu mgongoni humwitaje?

A. Kiduva B. Kibyongo

C. Kibogoyo D. Kibwiko

18. Tegua kitendawili: Ubwabwa wa mwana mtamu

A. Uyoga B. Usingizi

C. uji D. Ukufi

19. Sentensi ipi iliyo na matumizi sahihi ya -enye na -enyewe?

A. Kitabu chenye ninasoma kina picha chenyewe

B. Mtoto mwenye afya anatembea mwenyewe

C. Maneno yenye ulisema yenyewe nimeyasikia

D. Kwenye unasoma kwenyewe ni mbali

20. Ningekuwa na pesa ____ kitabu hiki.

A. ningalikinunua

B. ningekinunua

C. ningelinunua

D. nitakinunua

21. Zaibaki na Zuhura ni aina za ____

A. nauli B. majina

C. sayari D. wakristu

22. "Bonde la ufa" kwa wingi ni ____

A. Mabonde ya nyufa

B. Bonde za ufa

C. Mabonde za nyufa


D. Mabonde ya ufa

23. Moja kwa sita ni ____

A. thuluthi B. sudusi

C. humusi D. thumuni

24. Umbo hili ni ___



A. Mraba B. Duara

C. Mche duara D. Mstatili

25. Kanusha sentensi ifuatayo

**Mwalimu alituita sisi sote**

A. Mwanafunzi alitutuma sisi sote

B. Mwanafunzi hakutuita sisi sote

C. Mwalimu hakutuita sisi sote

D. Mwalimu hajatuita sisi sote

26. Chagua kiulizi sahihi

**Kuku huyu ni wa mtu ____?**

A. mgani B. gani

C. myupi D. wapi

27. Utaandikaje tarakimu 19699 kwa maneno?

A. Elfu kumi na tisa, mia tisa tisini na tisa

B. Kumi na sita elfu, mia sita tisini na sita

C. Kumi na tisa elfu, mia sita tisini na tisa

D. Elfu kumi na sita, mia sita tisini na sita

28. Uteo ni umoja wa neno ___

A. mauteo B. teo

C. viteo D. nyweo

29. Nyuga ni kwa mguu kama vile tarumbeta ni kwa

A. vidole B. mkono

C. mdomo D. macho

30. Kinyume cha nyuma ni mbele. Je, kinyume cha shiba ni ___

A. njaa B. kushiba

C. kula D. kutoshiba

***Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 31 - 40***

Jinsia ni hali ya kike au kiume. Zamani wakati neno usawa lilipokuwa halijapewa umuhimu, watu walikuwa na maoni tofauti kuhusu uana au jinsia na ubinadamu. Wengine walidhani kuwa mtoto wa kike ni bora kuliko wa kiume na wengine walidhani kuwa mtoto wa kiume ndiye bora zaidi.

Siku hizi mambo yamebadilika na fikra zimebadilika. Ukweli umepatikana. Ubora wa mtoto ni ubinadamu wake, tabia zake, akili zake na vitendo vyake bora maishani. Si ujinsia. Ubora haufuati ati labda ni mtoto wa kike au kiume. Wote ni sawa. Si ajabu kuwa watoto wa kike wanajua kutekeleza wajibu kwa unmakini na kuwajibika zaidi. Viongozi wa kike wanajua kutenda wajibu wao kwa umakini na kuwajibika zaidi.

Viongozi wa kike wanajua kutenda wajibu wao kwa uangalifu na uaminifu zaidi bila chelewa chelewa. Tuache ubaguzi wa jinsia. Binadamu wote ni sawa na wana haki sawa.

31. Zamani watu wengine walidhani kuwa ____
    A. kuna binadamu bora kuliko wengine
    B. wasichana na wavulana ni bora kuliko wazee
    C. watoto wa kike na wa kiume wote sawa
    D. kuna tofauti ya ubora kati ya watoto wa kike na wa kiume

32. Jinsia maana yake ni hali ya ____
    A. kuwa mtu wa kike
    B. mtu wa kiume
    C. kuwa mtu wa kike au kiume
    D. kuwa jinsia moja

33. Ukweli ambao umepatikana ni kwamba ____
    A. watoto wa kike na wa kiume wote ni sawa
    B. binadamu wote ni sawa
    C. watu wengine ni bora kuliko wenzao
    D. mambo yamebadilika

34. Kwa hakika, ubora wa binadamu hutegemea ____
    A. ujinsia B. umbo
    C. ubinadamu na utu D. sura

35. Katika habari hili neno jinsia kisawe chake ni ____
    A. Uana B. Jinsi
    C. Mtoto D. Usawa

36. Viongozi wa kike wamepewa sifa gani katika makala haya ____
    A. uzembe na chelewa chelewa
    B. umakini na kuajibika
    C. uangalifu na uaminifu
    D. ubaguzi na kuchelewa

37. Kutokana na sifa ya uangalifu tunampata mtu ____
    A. mwangalizi
    B. mwangalifu
    C. mwangavu
    D. mwangalivu

38. Taarifa inasema "Tuache ubaguzi wa jinsia". Maana yake hasa ni nini?
    A. tubaguane B. tutengane
    C. tuaminiane D. tuachane

39. Neno ubaguzi kinyume chake ____
    A. upendeleo B. upendo
    C. chuki D. usawa

40. Kichwa kisichofaa makala haya ni ____
    A. Ubaguzi wa jinsia
    B. Usawa wa jinsia
    C. Ubinadamu na jinsia
    D. Ubora wa jinsia

***Soma ufahamu ufuatayo kisha ujibu maswali 41 - 50***

Nidhamu ni hali ya kuwa tulivu na kukosa fitina. Ni jinsi ya kuonyesha heshima shuleni, nyumbani, kanisani na mahali popote pale. Wengi huchukulia kuwa nidhamu ni kuwa na bidii ya mchwa katika masomo. Sanasana wengi husema mtoto akiwa n… ıbari ya kwanza masomoni ana nidhamu.

Yeyote anaweza kuwa na nidhamu akiwa mwerevu au pia mjinga. Mtoto akiwaheshimu wakubwa wake na kufuata maagizo yaliyo ya manufaa hata awe ameshika mkia ana nidhamu. Wasichana na wavulana ndio wanakuwa watovu wa nidhamu sababu ya ujana. Ni jukumu la kila mmoja ulimwenguni kuwa na nidhamu. Mdogo siku hizi anaposalimiwa na mkubwa wake "u hali gani mwanangu?,"Vijana humjibu. "Poa buda". Mzee anaposalimia mtoto kwa heshima na kumwuliza mielekeo mbalimbali kwenye njia panda, mtoto husema "Buda, nenda kwa njia hiyo itakayokushow kwa akina ……"

Kwa nini siku hizi mambo yamekuwa hivi? Hakuna heshima katika mavazi. Wanawake wanavaa nguo zinazoona, wajipaka rangi midomoni ni kama paka aliyekunywa damu. Sketi zao ni fupi kupita kiasi, kifua wakiacha karibu wazi halafu kucha zao ndizo ndefu kuliko za <u>**mwewe**</u>. Je, dunia imepasuka mwonavyo? Tushirikianeni na tudumishe nidhamu kwa vizazi vijavyo.

41. Kulingana na ufahamu nidhamu ni nini?
    - A. Kuwa nambari moja darasani
    - B. Kuwa mtulivu na mwenye heshima
    - C. Kukosa heshima
    - D. Kuwa mfitini na mwana "sheng"

42. Kuwa na bidii ya mchwa ni
    - A. Kujikaza na kuwa na juhudi
    - B. Kupambana na maisha
    - C. Kuwa na nguvu
    - D. Kutumia maarifa na ujuzi

43. "Ameshika mkia…" Maana yake ni nini?
    - A. Kuamua kufanya jambo
    - B. Kuukamata mkia
    - C. Kuwa wa mwisho
    - D. kukunata mkiani kama kupe

44. Ni kikundi gani ambacho mwandishi anasema ni watovu wa nidhamu?
    - A. Mama na baba
    - B. Vijana na wasichana
    - C. Wasichana na wavulana
    - D. Wasichana na wanawali

45. Ni akina nani hujibu "poa…"
    - A. Mkubwa
    - B. Vijana
    - C. Wafupi
    - D. Wadogo

46. "Buda, nenda kwa njia hiyo itakayokushow kwa akina ……" Lugha hii huitwaje?
    - A. Kiswahili
    - B. Kiingereza
    - C. King'eng'e
    - D. Sheng

47. Ni gani haijatajwa kwenye ufahamu huu?
    - A. Nguo zinazoona
    - B. Vifua vitupu
    - C. Rangi midomoni
    - D. Rangi kuchani

48. Mwewe ni nani?
    - A. Aina ya nywele
    - B. Aina ya nyuni
    - C. Aina ya mnyama
    - D. Mzee sana

49. Vizazi vijavyo ni kama akina nani?
    - A. Nyanya
    - B. Babu
    - C. Vitukuu
    - D. Vitukutu

50. Taja kichwa kinachofaa katika ufahamu huu
    - A. Nidhamu inafaa
    - B. Maamkizi
    - C. Kuwa na bidii
    - D. Lugha chafu